# FUNZO LA 30

1. Ingawaje Mungu alituma mapigo tisa makali, je, Farao aliwaruhusu Waisraeli waondoke?
-La.

2. Je, pigo la mwisho ambalo Mungu alituma ni lipi?
-Pigo la mwisho litawaua wazaliwa wa kwanza wa Wamisri na mifugo yao.

3. Je, Mungu aliamuru kila jamii ya Israeli ifanye nini ili wazaliwa wao wa kwanza wasife?
-Wachague kondoo au mbuzi wa mwaka mmoja.

4. Je, ni aina gani ya kondoo au mbuzi ambayo Mungu aliwaamuru wachague ili wazaliwa wa kwanza wasife?
-Asiye na mawaa.

5. Je, kwa nini Mungu aliamuru kuwa huyo kondoo au mbuzi wa mwaka mmoja asiwe na mawaa?
-Kwa sababu Mungu ni mkamilifu.
-Kwa sababu kila anachosema Mungu ni kikamilifu.
-Kwa sababu kila anachofanya Mungu ni kikamilifu.

6. Katika siku ya kumi na nne, Mungu aliwaamuru Waisraeli wamfanyie nini yule kondoo?
-Mungu aliamuru kuwa kondoo lazima auawe.
-Mungu aliamuru kuwa kondoo lazima afe.

7. Je, kwa nini Mungu aliamuru kuwa kondoo lazima afe?



-Hii ilikuwa ili kuwafundisha Waisraeli kuwa adhabu ya dhambi ni kifo.

8. Je, Mungu aliwaamuru Waisraeli wafanye nini na damu ya yule kondoo?
-Waiteke kwa bakuli.

9. Je, Mungu aliwaamuru wafanyie nini ile damu watakoyoteka katika bakuli?
-Mungu aliwaamuru Waisraeli kwamba, wapake ile damu katika vizingiti vya mlango, upande wa juu na pande mbili za kando, katika kila nyumba ambapo yule mbuzi angeliwa.

10. Je, kwa nini Mungu aliamuru Waisraeli wawe ndani na damu iwe nje?
-Damu nje ilipaswa kuwafunika Waisraeli walio ndani.

11. Je, Mungu atatuuruhusu kujiokoa katika njia yetu?
-La.

12. Je, ni njia ya nani pekee ambayo itatuokoa?
-Njia ya Mungu.

13. Je, Mungu aliwaua wazaliwa wa kwanza wa Wamisri kama alivyoahidi?
-Ndiyo.

14. Baada ya wazaliwa wa kwanza wa Wamisri na wa Farao kufa, aliamua kufanya nini?
-Farao aliwaruhusu Waisraeli kuondoka.

Je, Farao au yeyote anaweza pigana na Mungu na ashinde?
-La.

-Baada ya Mungu kuwaongoza Waisraeli kutoka Misri, aliwaelekeza katika nchi gani?

-Kurejea kwa nchi ya Kanaani.

-Kanaani ilikuwa nchi ambayo Mungu aliahidi Ibrahamu, Isaka na Yakobo.

-Waisraeli walipoenda Misri hapo mwanzo, walikuwa watu 70.

-Sasa, baada ya kuishi miaka 400, walikua watu milioni mbili.

-Je, Mungu aliwezaje kuongoza watu milioni mbili?

Tusome Kutoka 13:21-22

21-Bwana naye akawatangulia mchana ndani ya wingu mfano wa nguzo, ili awaongoze njia; na usiku, ndani ya moto mfano wa nguzo, ili kuwapa nuru; wapate kusafiri mchana na usiku;

22-ile nguzo ya wingu haikuondoka mchana, wala ile nguzo ya moto haikuondoka usiku, mbele ya hao watu.

-Je, Mungu aliwaongoza vipi Waisraeli mchana?
-Kwa wingu.

-Je, Mungu aliwaongoza vipi Waisraeli usiku?



-Kwa nguzo ya moto.

-Je, kama Mungu hangewaongoza Waisraeli, wangejua walikopaswa kwenda?
-La.

-Je, kama Mungu hangewaongoza Waisraeli, nini kingewafanyikia?

-Wangepotea na kufa.

-Kwa sababu Mungu aliwapenda Waisraeli, aliwaongoza ili wasipotee na kufa.

-Mungu aliwaongoza Waisraeli kuelekea kwa bahari iitwayo Bahari ya Shamu.

-Katika Bahari ya Shamu, Mungu aliwaambia Waisraeli wapumzike kwa muda.

Tusome Kutoka 14:1-3

1-Bwana akasema na Musa, akamwambia,

2-Waambie wana wa Israeli, kwamba warudi na kupiga kambi yao mbele ya Pi-hahirothi, kati ya Migdoli na bahari, kukabili Baal-sefoni; mtapanga mbele yake karibu na bahari.

3-Naye Farao atasema katika habari za wana wa Israeli, Wametatanishwa katika nchi, ile jangwa imewazuia wasitoke.

-Je, kwa nini Mungu aliwaongoza Waisraeli kwenda kando ya Bahari ya Shamu?

-Mungu alitaka kuwaonyesha Waisraeli na Wamisri kuwa yeye pekee ndiye Mungu.

-Je, ni nani aliyemwambia Mungu alichofikiria Farao?
-Hakuna.

-Je, Mungu alijuaje alichofikiria Farao?

-Mungu alijua kila wazo alilofikiria Farao kabla hajalifikiria.
-Mungu anayajua mawazo yetu kabla tuyafikirie.

-Tusikilize alichosema Farao:

Tusome Kutoka 14:5-9

5-Mfalme wa Misri aliambiwa ya kuwa wale watu wamekwisha kimbia; na moyo wa Farao, na mioyo ya watumishi wake, iligeuzwa iwe kinyume cha hao watu, nao wakasema, Ni nini jambo hili tulilotenda, kwa kuwaacha Waisraeli waende zao wasitutumikie tena?
6-Akaandalia gari lake, akawachukua watu wake pamoja naye;
7-tena akatwaa magari mia sita yaliyochaguliwa, na magari yote ya Wamisri, na maakida juu ya magari hayo yote.
8-Na Bwana akaufanya moyo wake Farao mfalme wa Misri kuwa mgumu, naye akawafuata wana wa Israeli; kwa sababu wana wa Israeli walitoka kwa ujeuri.



9-Wamisri wakafuata nyuma yao, farasi zote na magari yote ya Farao, na askari wake wenye kupanda farasi, na jeshi lake, nao wakawapata hali wamepanga pale karibu na bahari, karibu na Pi-hahirothi, kukabili Baal-sefoni.

-Farao alifikiria kuwachukua mateka Waisraeli tena.

-Kwa hivyo, Farao alikusanya majeshi yake na wakaelekea kuwachukua mateka Waisraeli.

-Je, ni nani aliyekuwa akiongoza Farao kwenda kuwachukua mateka Isaraeli?

-Shetani.

-Je, kwa nini Shetani alitaka Farao achukue Israeli mateka?

-Kwa sababu Shetani alitaka kuharibu Israeli.

-Je, Israeli walifanya nini walipoona Farao akija kuwachukua mateka?

Tusome Kutoka 14:10a & 11-12

10-Hata Farao alipokaribia, wana wa Israeli wakainua macho yao, na tazama, Wamisri wanakuja nyuma yao; wakaogopa sana;
11-Wakamwambia Musa, Je! Kwa sababu hapakuwa na makaburi katika Misri umetutoa huko ili tufe jangwani? Mbona umetutendea haya, kututoa katika nchi ya Misri?

12-Neno hili silo tulilokuambia huko Misri, tukisema, Tuache tuwatumikie Wamisri? Maana ni afadhali kuwatumikia Wamisri kuliko kufa jangwani.

-Waisraeli walimlaumu Musa, na wakatamani kuwa hawangetoka Misri.

-Ingawaje Waisraeli waliona Mungu alivyotuma yale mapigo kumi, bado hawakumuamini Mungu.

-Waisraeli hawakumuamini Mungu, lakini Musa alimuamini Mungu.

-Hiki ndicho alichosema Musa:

Tusome Kutoka 14:13-14

13-Musa akawaambia watu, Msiogope, simameni tu, mkauone wokovu wa Bwana atakaowafanyia leo; kwa maana hao Wamisri mliowaona leo hamtawaona tena milele.
14-Bwana atawapigania ninyi, nanyi mtanyamaza kimya.

-Je, Waisraeli waliweza kujiokoa?
-La.

-Je, kwa nini Waisraeli hawangeweza kujiokoa?

-Kwa kuwa Bahari ya Shamu ilikuwa mbele yao, kando ilikuwa milima na nyuma Farao na jeshi lake waliwaandama.



-Waisraeli walikuwa katika mtego.

-Je, ni nani pekee aliyeweza kuwaokoa Waisraeli?
-Mungu.

-Adamu na Hawa walipoondolewa katika Bustani ya Edeni, hawakuweza kurejea.

-Ni Mungu tu aliyeweza kufanya njia ya kuwaokoa.

-Mikono na miguu ya Isaka ilipofungwa na kisu kimeinuliwa ni Mungu pekee aliyeweza kumuokoa Isaka.

-Ni Mungu pekee aliyeweza kufanya njia ya kumuokoa Isaka.

-Sasa, Waisraeli walikuwa wametegwa, hawangeweza kujiokoa.

-Ni Mungu pekee ambaye angefanya njia ya kuwaokoa.

-Kama vile ni Mungu tu aliyeweza kufanya njia ya kuwaokoa Waisraeli, ni yeye pekee anayeweza kutuokoa.

-Je, Mungu alifanya njia ya kuwaokoa Waisraeli?

Tusome Kutoka 14:21-22

21-Musa, akanyosha mkono wake juu ya bahari; Bwana akaifanya bahari irudi nyuma kwa upepo wa nguvu utokao mashariki, usiku kucha, akaifanya bahari kuwa nchi kavu, maji

yakagawanyika.

22-Wana wa Israeli wakaenda ndani kati ya bahari katika nchi kavu; nayo maji yalikuwa ukuta kwao mkono wa kuume, na mkono wa kushoto.

-Mungu aliamuru Bahari ya Shamu ipasuke na Waisraeli wakapita katika njia kavu.

-Je, ilikuwa vigumu kwa Mungu kuipasua Bahari ya Shamu?
-La.

-Je, kwa nini haikuwa vigumu kwa Mungu kuipasua Bahari ya Shamu?

-Kwa sababu Mungu aliumba Bahari ya Shamu.
-Kwa sababu Mungu ni Bwana wa bahari zote.

-Kwa sababu Mungu ni mwenye nguvu zote na anaweza fanya chochote.

-Waisraeli walianza kuvuka  Bahari ya Shamu.

-Farao na jeshi lake waliwafuata ili kuwateka Israeli, je Mungu alifanya nini ili kulinda Israeli?

Tusome Kutoka 14:19-20

19-Kisha malaika wa Mungu, aliyetangulia mbele ya jeshi la Israeli, akaondoka akaenda nyuma yao; na ile nguzo ya wingu ikaondoka hapo mbele yao, ikasimama nyuma yao;



20-ikafika kati ya jeshi la Misri na jeshi la Israeli; napo palikuwa na lile wingu na lile giza, lakini lilitoa nuru wakati wa usiku; na hawa hawakuwakaribia hawa usiku kucha.

-Mungu aliweka wingu katikati ya Waisraeli na Farao na majeshi yake.

-Hili wingu liliangazia Israeli na kufanya giza kwa Wamisri.

-Ingawaje hilo wingu lilifanya giza kwa Wamisri, walizidi kuwafuata Waisraeli.

-Farao na jeshi lake waliwafuata Waisraeli kwenda katika Bahari ya Shamu.

Tusome Kutoka 14:23

23-Na wale Wamisri wakawafuatia, wakaingia ndani kati ya bahari, farasi zote za Farao, na magari yake, na wapanda farasi wake.

-Je Mungu alimfanyia nini Farao alipowafuata Waisraeli ndani ya Bahari ya Shamu?

Tusome Kutoka 14:24-28

24-Ikawa katika zamu ya alfajiri, Bwana akalichungulia jeshi la Wamisri katika ile nguzo ya moto na ya wingu, akalifadhaisha jeshi la Wamisri.

25-Akayaondoa magurudumu ya magari yao, hata yakaenda kwa uzito; na Wamisri wakasema, Na tukimbie mbele ya Israeli; kwa sababu Bwana anawapigania, kinyume cha Wamisri.

26-Bwana akamwambia Musa, Nyosha mkono wako juu ya bahari, ili maji yarudi tena juu ya Wamisri, juu ya magari yao, na juu ya farasi zao.

27-Musa akaunyosha mkono wake juu ya bahari, na kulipopambazuka, bahari ikarudi kwa nguvu zake; Wamisri wakakimbia mbele yake; na Bwana akawakukutia mbali hao Wamisri kati ya bahari.

28-Yale maji yakarudi yakafunikiza magari na wapanda farasi, hata jeshi lote la Farao lililoingia katika bahari nyuma yao; hakusalia hata mtu mmoja.

-Mungu aliwazamisha Farao na majeshi yake katika Bahari ya Shamu.

-Hakuna hata mmoja aliyesalia.

-Je, Farao alipigana dhidi ya Mungu na akashinda?
-La.

-Je, ni nani anayeweza kupigana dhidi ya Mungu na ashinde?
-Hakuna.

-Je, kuna Waisraeli waliokufa?

Tusome Kutoka 14:29-30



29-Lakini wana wa Israeli wakaenda katika nchi kavu katikati ya bahari; na hayo maji yalikuwa ni kuta upande wao wa kuume, na upande wao wa kushoto.

30-Ndivyo Bwana alivyowaokoa Israeli siku ile mikononi mwa Wamisri; Waisraeli wakawaona Wamisri ufuoni kwa bahari, wamekufa.

-Hakuna aliyekufa katika Israeli.

-Je, kwa nini hakuna aliyekufa katika Israeli?

-Kwa sababu Mungu aliwalinda.

-Je, kwa nini Mungu aliwalinda Israeli?

-Kwa sababu Mungu aliahidi kumtuma Mwokozi kupitia kwa Ibrahamu na Waisraeli.

-Kwa sababu pia Mungu alipanga kutuma Biblia yake kupitia kwa Ibrahamu na Israeli.

-Tukimuamini Mungu, atatuokoa.

-Kama hatutamuamini Mungu, hawezi kutuokoa.